SUMAIT University Journal (SUJ)
eissn (2953-2698)
Issue No.16 June 2025

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO WA USAJILI WA CHAKULA JUU YA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA VIFUNGASHIO VYA BIDHAA

Twaiba A. Omar (phD)
thuwaibaomar2021@gmail.com
Department of Swahili,
School of Swahili and Foreign Languages,
Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA
Haroun A. Maalim(phD)
Haroun.maalim@gmail.com
School of Swahili and Foreign Languages,
Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA)

Mahmo ud Yussuf Haji(phD)
School of Swahili and Foreign Languages,
Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA)

Received: January 2025, Accepted: April 2025, published: June 2025
© SUMAIT University Journal 2025

Abstract:

The article has assessed the guideline of registration of Pre Packaged Food (Nov, 2018) in the language use item in product packaging in Zanzibar. Food product packaging in Zanzibar uses various languages for instructions concerning the item. Data of this article has been derived through text analysis and interrogation supervisor implementing the guideline. The research sample consists of products manufactured in Tanzania. This theory of language usage program initiated by Ruiz in 1984 which leads data analysis in this research. This theory has three pillors which are used. The result of this investigation show that out of 20 food products packaging, it is only 16 products packaging use the language program initiated however most product packaging in English language because of English hegemony. According to the result of this investigation I suggest the authority concerned to give out enough education and take the best measure for all who go opposite of the guideline instructions on the language use in products packaging.

Ikisiri:

Makala hii imetathmini utekelezajiwa mwongozo wa usajili wa bidhaa za chakula (Nov,2018) juu ya kipengele cha matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa. Vifugashio vya bidhaa za chakula Zanzibar, hutumia lugha mbalimbali kutoa maelekezo yanayotokana na bidhaa husika. Data za makala hii zimepatikana kwa kutumia mbinu ya uchambuzi matini na usaili kwa wasimamizi wa utekelezaji wa mwongozo. Sampuli ya utafiti huu ni vifungashio 20 vya bidhaa zinazotengenezwa Tanzania. Nadharia ya mazingatio ya mpango lugha iliyoasisiwa na Ruiz (1984) ndio iliyoongoza uchambuzi wa data za utafiti huu. Nadharia hii ina misingi mitatu ambayo yote imetumika katika uchambuzi wa data za makala hii. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa, vifungashio 16 kati ya

20 vilivyochunguzwa ambapo ni sawa na asilimia 80 vimetekeleza agizo la mwongozo juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula. Zaidi ya hayo, kushika hatamu kwa lugha ya Kiingereza duniani kumesababisha vifungashio vingi vya bidhaa ziliopo Zanzibar kutumia lugha ya Kiingereza. Kutokana na matokeo ya utafiti huu napendekeza kuwa, mamlaka husika itoe elimu ya kutosha pamoja na kuwachukulia hatua, wale wote wanaokiuka agizo la mwongozo juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa.

Keywords: **Tathmini, Utekelezaji, Mwongozo, Chakula, Bidhaa na Vifungashio**

1. UTANGULIZI

Makala hii inahusu tathmini ya utekelezaji wa mwongozo wa usajili wa chakula, katika kipengele cha matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula. Makala hii, imegawiwa katika sehemu tano ambazo ni: utangulizi, mbinu za utafiti, uwasilishaji na uchambuzi wa data, matokeo ya utafiti na hitimisho. Tunapozungumzia, dhana ya mwongozo wa usajili wa chakula, ni maelekezo yanayotakiwa kufuatwa juu ya utumiaji wa lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula, Lengo la kuwekwa kipengele hiki ni kumsaidia mtumiaji wa bidhaa husika kujua maelekezo mbalimbali kama vile, namna bidhaa ilivyotengenezwa kwa kuzingatia viambata vyake, matumizi, uhifadhi na muda wa kutumia. Jambo hili, limetupa ari ya kuona kuwa, kuna haja ya kufanya utafiti wa kuangalia tathmini ya utekelezaji wa kipengele hicho muhimu kwa mtumiaji wa bidhaa. Tunapoangalia tathmini ya utekelezaji wa mwongozo wa usajili, tunakusudia kuangalia ni kwa kiasi gani mtayarishaji wa bidhaa anazingatia, kutii na kufuata maelekezo juu ya suala zima la matumizi ya lugha, zinazostahiki kutumika katika vifungashio kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa katika mwongozo wa usajili wa bidhaa za chakula kwa upande wa Zanzibar. Uchambuzi wa kipengele cha lugha katika mwongozo na utekelezaji wake, umefanyiwa kazi na wataalamu na watafiti mbalimbali katika sehemu tofauti duniani. Hali hii inatupa fursa ya kudurusu kazi zao kabla ya kuingia katika lengo la makala hii.

2. MATUMIZI YA LUGHA KATIKA VIFUNGASHIO VYA BIDHAA

Wataalamu mbalimbali wamezungumzia matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa. Miongoni mwao ni [15] ambao wamechunguza matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa kwa kuzingatia mitazamo ya watumiaji wa bidhaa wa Kichina. Katika utafiti huo wamegundua kuwa, watumiaji wa Kichina wanapendelea zaidi bidhaa ambazo vifungashio vyake hutumia lugha zao za asili kuliko lugha za kigeni. Matumizi hayo ya lugha ya asili katika vifungashio vya bidhaa ni miongoni mwa utekelezaji wa mwongozo/sera ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa. Mara nyingi sera/miongozo inayofafanua matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa hutumia lugha moja wapo ya kigeni kwa kuipa kipaumbele katika sera hiyo. Kawaida, taifa linapoweka lugha ya pili na lugha hiyo ikawa ya kigeni katika miongozo hiyo, utekelezaji wake huathiri sana vifungashio vya bidhaa [6]. Wakifafanua zaidi wanaeleza kuwa, kutoa fursa ya kuchagua lugha ya wenyeji na lugha ya kigeni husababisha wazaalishaji wa bidhaa na watumiaji wa bidhaa kupendelea zaidi bidhaa zilizotumia lugha ya kigeni.

[9] wanaeleza kuwa, katika utekelezaji wa mwongozo/sera ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa, nchini Ujerumani hutumia lugha mbalimbali kama vile, Kijerumani, Kifaransa, Kiingereza, Kispanishi na Kidutchi kama sehemu ya utekelezaji wa sera ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa. Wataalamu hao, wanaeleza kuwa, Wajerumani hufanya hivyo kwa sababu bidhaa zao husambazwa zaidi katika nchi ambazo hutumia lugha hizo. Zaidi ya hayo, bidhaa inapotumia lugha zaidi ya moja huwa na soko zaidi kimataifa. Maelezo haya yanathibitisha kuwa, Wajerumani hutumia lugha tofauti katika vifungashio vya bidhaa zao ikiwemo Kijerumani. Pia, wataalamu hao wanasisitiza kuwa, jambo hilo halikuwa likitokea kwa bahati mbaya, bali ilikuwa ni utekelezaji wa sera ya jamii hiyo. Hivyo, ni wazi kuwa, watayarishaji wa bidhaa wanatakiwa kuwa makini kufuata miongozo kama hiyo ili kufikia lengo la jamii na kufikia maendeleo ya kweli.

Wazalishaji wa bidhaa wengi nchini China hutekeleza Mwongozom wa utumiaji wa lugha katika vifungashio vya bidhaa kwa kutumia zaidi lugha zao za asili kwa zile bidhaa za ndani. Aidha, wazalishaji hao hutumia lugha zao za asili sambamba na lugha nyingine za kigeni kwa bidhaa ambazo hutoka nje ya China. Wafanya biashara wengi nchini humo wamekuwa wakitumia lugha ya Kichina katika vifungashio vya bidhaa zao. Hii ni kutokana na kuwa lugha hii imepewa kipaumbele zaidi kuliko lugha ya Kiingereza nchini humo hususan katika bidhaa ambazo hutumiwa zaidi ndani ya China. Andiko hili limesaidia utafiti huu kuona namna Wachina wanavyotekeleza sera na miongozo juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa [4 na 23].

Maelezo ya wataalamu hawa yameonesha sababu mbili kuu za matumizi ya lugha zao katika vifungashio vya bidhaa. Mosi, kuzipa hadhi lugha za wenyeji ili ziweze kustawi na kunawiri. Pili, matumizi hayo yanashajiisha uelewa wa maelekezo yanayotokana na bidhaa husika. Hali hii huwa inatanabahisha walaji kuelewa bidhaa wanayoitumia.

[8] Katika utafiti wao wamelinganisha matumizi ya lugha ya Kiingereza na lugha za Kienyeji nchini Pakistani. Katika utafiti huo wamegundua kuwa, wafanya biashara nchini humo wanapendelea zaidi matumizi ya lugha yao ya asili katika vifungashio vya bidhaa. Ikiwa ni miongoni mwa utekelezaji wa sera ya nchi hiyo juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa. Nchini Palestina watayarishaji wa bidhaa hutumia zaidi lugha yao ya Kiarabu kama lugha ya taifa na lugha rasmi. Sambamba na hayo, vifungashio vya bidhaa nchini humo hutumia zaidi lugha yao ya asili ambayo ni Kiarabu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya lugha za vifungashio vya bidhaa. Aidha, vifungashio vya bidhaa nchini humo hutumia lugha mbalimbali ikiwemo Kiingereza. Hata hivyo, lugha ya Kiingereza hutumika zaidi kwa zile bidhaa ambazo zinatarajiwa kuuzwa nje ya nchi ikiambatana na lugha ya Kiarabu [16].

amechunguza matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa kwa kuzingatia mitazamo ya watumiaji wa bidhaa zinazotengezwa Malaysia. Katika utafiti huo, amegundua kuwa, watumiaji wa bidhaa nchini Malaysia wanapendelea zaidi bidhaa ambazo vifungashio vyake hutumia lugha zao za asili kuliko lugha za kigeni kama sehemu ya utekelezaji wa sera ya lugha za vifungashio nchini humo[23].

Utafiti uliochunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika vifungashio vya bidhaa za watoto nchini Tanzania, umegundua kuwa, katika utekelezaji wa mwongozo watayarishaji wa bidhaa za watoto jijini Dodoma, hutumia zaidi lugha ya Kiingereza kuliko lugha nyingine ikifuatiwa na Kifaransa, Kiarabu, Kichina na Kituruki. Hali inayoonesha ukiukwaji wa utekelezaji wa kipengele cha sera ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za watoto kama vile maziwa na unga wa lishe. Aidha, mwongozo wa usajili wa chakula katika kipengele cha matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za watoto Tanzania bara umeagiza kuwa, bidhaa za watoto ziandikwe kwa kutumia lugha ya Kiswahili lakini maagizo hayo hayatekelezwi ipasavyo na badala yake, bidhaa hizo hutumia zaidi lugha za kigeni [1].

Baadhi ya wafanya biashara hukumbana na changamoto zinazohusiana na utekelezaji wa sera juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa, hasa kwa wazalishaji wadogo ambao wanaweza kukosa rasilimali za kutosha kutekeleza masharti hayo. Gharama za kuongeza tafsiri na uchapaji wa vifungashio kwa lugha mbalimbali zinaweza kuwa mzigo mzito kwa baadhi ya wafanya biashara, hasa katika soko la bidhaa za bei nafuu [12].

Mambo ya msingi tuliyoyabaini katika kazi tangulizi ni kuwa, kazi zao zimeonesha namna watayarishaji wa bidhaa wanavyotumia lugha za asili na za kigeni katika utekelezaji wa sera katika kipengele cha lugha za vifungashio vya bidhaa. Jambo ambalo husaidia kukamilisha suala la mawasiliano baina ya mtumiaji wa bidhaa na mtayarishaji wa bidhaa hizo. Matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa humsaidia mtumiaji kufahamu maelekezo ya bidhaa husika. Pia, matumizi ya lugha hizo katika bidhaa huwa yanalenga kutekeleza sera za lugha za nchi husika. Hata hivyo, kwa Tanzania na Zanzibar lugha ya Kiingereza hutumika zaidi kutokana na kushika hatamu kwa lugha hiyo katika soko la biashara duniani, pamoja na mabaki ya kikoloni na kuona lugha ya Kiingereza ndio ustaarabu wa kijamii. Kazi hizi zimezingatia zaidi matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa kama ni sehemu ya utekelezaji wa sera husika. Hali ambayo imempa ari mtafiti wa utafiti huu, kutathimini utekelezaji wa sera/mwongozo wa usajili wa chakula, katika kipengele cha matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula, Zanzibar.

3.0 METHODOLOJIA YA UTAFITI

Makala hii imetumia mkabala wa kitaamuli. Mbinu ya kimaelezo imetumika katika uwasilishaji na uchambuzi wa data. Utafiti huu, umefanyika uwandani na maktabani. Mbinu zilizotumika ni usaili na uchambuzi matini katika ukusanyaji wa data husika. Utafiti huu, umejikita katika eneo la Zanzibar. Sampuli ya utafiti huu ni vifungashio 20 vya bidhaa zinazotengezwa Tanzania, ambapo mtafiti alitumia usampulishaji nasibu kupata vifungashio vya bidhaa za chakula. Aidha, watoa taarifa wanne ambao ni miongoni mwa wasimamizi wa utekelezaji wa mwongozo wa usajili wa chakula ni miongoni mwa sampuli iliyotumika ambapo mtafiti alitumia usampulishaji lengwa kuwapata watoa taarifa hao. Hatua ambazo zimemuwezesha mtafiti kupata data zinazoonesha utekelezwaji wa mwongozo husika. Jambo ambalo limemwongoza mtafiti kutathmini utekelezwaji wa kipengele namba 5.3. 11. (b) cha mwongozo juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula.

4.0 UTEKELEZWAJI WA MUONGOZO

Mwongozo wa usajili wa chakula, wa Zanzibar, upo kisheria ili kukidhi mahitaji ya kijamii na kiuchumi. Mwongozo huo umetoa fursa mbalimbali na mipaka kwa wafanya biashara kutumia lugha tofauti katika vifungashio vya bidhaa zinazozalishwa na hata zile zinazoingizwa kutoka nje. Kipengele namba 5.3. 11. (b) cha mwongozo kinaeleza kuwa:

"Any statement, information or declaration that is required by any requirement under these guidelines to appear on the label of any prepackage food shall be in Swahili or English or both Kiswahili and English, or any other language with either Swahili or English". (chanzo: Mwongozo wa usajili wa chakula, Nov.2018).

> *"Taarifa yoyote au tamko ambalo linahitajika katika kukamilisha masharti yoyote chini ya miongozo hii ambayo inahitajika kuwepo kwenye vifungashio vya chakula chochote kilichowekwa tayari itakuwa katika Kiswahili au Kiingereza au Kiswahili na Kiingereza, au lugha nyingine yoyote pamoja na Kiswahili au Kiingereza" (tafsiri yangu).*

Kwa mujibu wa mwongozo huo vifungashio vya bidhaa za chakula vinaweza kutumia lugha ya Kiswahili au Kiingereza au Kiswahili na Kiingereza au Kiswahili na lugha nyingine au Kiingereza na lugha nyingine. Hivyo, makala hii imenuwia kutathmini utekelezwaji wa agizo la mwongozo kwa watayarishaji wa bidhaa juu ya kipengele cha matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa. Kwa mujibu wa mwongozo, vifungashio ambavyo vimetekeleza agizo la mwongozo juu ya matumizi ya lugha ni vile vifungashio ambavyo vimetumia lugha ya Kiswahili pekee, Kiingereza pekee, Kiswahili na Kiingereza, Kiswahili na lugha nyingine ya kigeni, pamoja na Kiingereza sambamba na lugha nyingine ya kigeni. Uchambuzi wa makundi hayo umefafanuliwa kwa kuzingatia aina ya kundi husika, sambamba na maelekezo ya mwongozo wa usajili juu ya kipengele cha matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa.

4.1 VIFUNGASHIO VYA BIDHAA ZA CHAKULA VILIVYOTUMIA LUGHA YA KISWAHILI

Kutumika kwa Kiswahili pekee katika vifungashio vya bidhaa ziliopo Zanzibar, ni fursa halali iliyotolewa na mwongozo wa usajili wa chakula wa Zanzibar. Hivyo, matumizi hayo ni miongoni mwa utekelezwaji wa mwongozo wa usajili wa bidhaa za chakula Zanzibar juu ya kipengele cha lugha katika vifungashio vya bidhaa. Vifungashio vya bidhaa vilivyobainika kutumia Kiswahili pekee ni vichache ukilinganisha na vile vilivyotumia Kiingereza pekee. Data ifuatayo ni mfano wa bidhaa ya chakula iliyotumia lugha ya Kiswahili.

Mfano wa bidhaa yenye kifungashio kilichoandikwa kwa lugha ya Kiswahili

Data hii inaonesha kuwa, kifungashio hiki cha bidhaa ya kahawa kimetumia lugha ya Kiswahili tu. Kupitia mbinu ya uchambuzi matini, utafiti umegundua kuwa, vifungashio vya bidhaa vilivyotumia Kiswahili pekee ni adimu Zanzibar. Pamoja na hali hiyo, kifungashio hiki kimekwenda sambamba na maelekezo yaliyopo katika mwongozo wa usajili wa chakula Zanzibar. Kipengele namba 5.3.11 (b) cha mwongozo wa usajili wa chakula kimeweka bayana matumizi ya lugha ya Kiswahili pekee katika vifungashio vya bidhaa za ndani na zile zinazotoka nje.

Kupitia mbinu ya uchambuzi matini utafiti umebaini kuwa, kati ya vifungashio 20 vilivyochunguzwa, vifungashio viwili sawa na 10% ndivyo vilivyotumia lugha ya Kiswahili pekee. Hii ni kutokana na hatamu ya lugha ya Kiingereza hususan katika soko la biashara kitaifa na kimataifa. Vifungashio hivyo ni miongoni mwa vifungashio vya bidhaa vinavyofuata utekelezaji wa agizo la mwongozo wa usajili wa chakula juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio hivyo. Zaidi ya hayo, vifungashio vilivyotumia lugha ya Kiswahili pekee mbali ya kufuata mwongozo lakini pia ni vifungashio vilivyokuwa bora kwa jamii ya watu wa Zanzibar. Hii ni kutokana na kutumia lugha ya Kiswahili. Lugha ambayo ni ya kwanza na ya taifa kwa Wazanzibari. Zaidi ya hayo, ni miongoni mwa lugha zilizosisitizwa katika mwongozo kutumika katika vifungashio vya bidhaa.

Suala la kutumia lugha ya Kiswahili pekee katika vifungashio, ni suala lililoelekezwa katika mwongozo pale uliposema kuwa, "*... katika Kiswahili au Kiingereza au Kiswahili na*.." Jambo, hili limejenga ubora wa kifungashio hiki katika matumizi ya lugha. Hivyo, ni wazi kuwa, utumiaji wa lugha ya Kiswahili katika vifungashio ni utumiaji wa rasilimali hiyo muhimu kwa jamii ya Wazanzibari. Umuhimu wake unatokana na watumiaji wa bidhaa hizo kuweza kufahamu maelekezo ya bidhaa husika. Aidha, kupitia mbinu ya mahojiano wasimamizi wa utekelezwaji walikiri kuwa, kutumia lugha ya Kiswahili pekee katika vifungashio vya bidhaa ni utekelezwaji wa agizo la mwongozo huo. Zaidi ya hayo, wamedai kuwa licha ya kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha mama kwa Wazanzibari lakini bado wafanya biashara wenyeji hupendelea zaidi kutumia lugha ya Kiingereza

kuliko Kiswahili. Jambo ambalo limepelekea uhaba mkubwa mno wa vifungashio vinavyotumia lugha ya Kiswahili.

Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika vifungashio vya bidhaa ni rasilimali muhimu kwa jamii. Hoja hii inaungwa mkono [13] pale aliposema kuwa, lugha ni rasilimali muhimu ambayo inamuwezesha mwanajamii kutatua changamoto mbalimbali anazokumbana nazo katika maisha ya kila siku. Hivyo, lugha inayofahamika katika jamii ni nyenzo muhimu katika kufanikisha na kuboresha shughuli za maisha kwa mwanaadamu.

Matokeo ya utafiti huu yanafanana na utafiti wa [1] alioufanya jijini Dodoma. Katika utafiti wake amegundua kuwa, vifungashio vya bidhaa za watoto zinazozalishwa jijini humo hutumia zaidi lugha ya Kiingereza na lugha nyingine za kigeni kuliko lugha ya Kiswahili. Kitendo ambacho kinakwenda kinyume na agizo la mwongozo husika. Jambo ambalo limepelekea uchache mno kwa vifungashio vya bidhaa vinavyotumia lugha ya Kiswahili. Mtafiti huyu amesema kuwa, ingelifaa taarifa muhimu zilizo katika vifungashio vya bidhaa za watoto ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha inayofahamika na jamii pana. Hii ni kwa sababu lugha ya Kiswahili ni lugha ya wenyeji, na wazawa wa Tanzania. Hivyo, kutumika kwake ni kutumika kwa rasilimali muhimu kwa jamii ya watumiaji wa bidhaa hizo. Zaidi ya hayo matumizi hayo ni sehemu ya utekelezwaji wa mwongozo husika. Hoja hii inatilia mkazo juu ya lugha za wenyeji kutumika katika vifungashio vya bidhaa.

Matumizi ya lugha za wenyeji katika vifungashio vya bidhaa yanaungwa mkono na tafiti mbalimbali zilizofanywa na [4], [8] na [16] ambao wamedai kuwa, matumizi ya lugha za asili ni muhimu katika vifungashio vya bidhaa. Zaidi ya hayo wameeleza kuwa, matumizi ya lugha za kienyeji hususan katika bidhaa zinazotumika ndani ya nchi ni jambo jema kutokana na kuweza kufahamika na wenyeji ambao pia ni watumiaji wakubwa wa bidhaa hizo. Wakizungumzia kuhusu matumizi ya lugha za wenyeji kwa soko la nje, watafiti hao wamedai kuwa lugha za wenyeji pia zina nafasi kupitia mambo mawili makuu nayo ni; soko la biashara pamoja na utambulisho wa taifa linalozalisha bidhaa hiyo. Kupitia mtaalamu huyu tunaona kuwwa matumizi ya lugha ya wenyeji na wageni katika vifungashio vya bidhaa yana faida mbili kuu. Mosi kuwafahamisha watumiaji wa bidhaa mambo muhimu yanayohusu bidhaa husika, lakini pia utumiaji wa lugha hizo ni sehemu ya utekelezwaji wa sera zao juu ya matumizi ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa.

Aidha, kutumika kwa lugha za wenyeji ni utiliaji mkazo wa matumizi ya lugha inayoeleweka na jamii pana. Hoja ambayo ina ungwa mkono na wataalamu mbalimbali kama vile, [18] na [7] wakiitolea mfano Amerika ya Kaskazini wameeleza kuwa, biashara nyingi za kimataifa hutengeneza lebo zao kwa kutumia mchanganyiko wa Kiingereza, Kihispania na Kifaransa (au zote tatu). Hii inamaanisha kuwa, wanaweza kusafirisha bidhaa popote ndani ya Amerika Kaskazini, kwani, hizo ndizo lugha tatu zinazozungumzwa na kufahamika zaidi katika nchi hizo. Akitilia mkazo hoja hiyo [17] amedai kuwa, matumizi ya lugha za wenyeji ni muhimu katika kuendeleza uchumi na maendeleo ya taifa. Akifafanua zaidi amedai kuwa, kwa mujibu wa sera ya elimu ya mwaka 2014 lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa na inatumika kama lugha ya kwanza au ya pili kwa wananchi wengi nchini Tanzania. Lugha ya Kiswahili imekua kwa kiwango cha kimataifa ambapo inaweza kutumiwa na wananchi

wengi kupata maarifa na ujuzi katika nyanja mbalimbali, ikiwa ni pamoja na biashara, Sayansi na teknolojia.

Naye, [2] amedai kuwa, lugha za wenyeji zinahitaji kukuzwa na kuendelezwa kwa sababu ndizo zinazozungumzwa na asilimia kubwa ya jamii za Kiafrika. Vilevile, lugha asilia huhitaji kutumika ili kufikia malengo ya maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kiutawala katika jamii. Kwa maana hiyo lugha ya Kiswahili kutumika katika vifungashio vya bidhaa ni njia moja wapo ya ufikiaji wa malengo ya kufahamu maelekezo ya bidhaa kwa watumiaji wa bidhaa.

Matumizi ya lugha ya Kiswahili ni muhimu katika vifungashio vya bidhaa zinazotengezwa na kuingizwa Zanzibar. Hii ni kutokana na uhalisia wa watu wa Zanzibar na maisha yao.

4.2 VIFUNGASHIO VYA BIDHAA ZA CHAKULA VILIVYOTUMIA LUGHA YA KIINGEREZA

Matumizi ya lugha ya Kiingereza katika vifungashio vya bidhaa yamebainika katika vifungashio vya bidhaa zinazozalishwa Tanzania. Hali hii, inatokana na kuwa, Kiingereza ni lugha ya kitaifa na kimataifa inayokubalika katika ulimwengu wa biashara. Bidhaa kama vile vinywaji na chakula kilichofungashwa vimebainika mara nyingi hutumia Kiingereza zaidi katika vifungashio kwa kuwa, ni lugha inayojulikana na inatumiwa sana katika muktadha wa kimataifa na ulimwengu wa biashara.

Tanzania sio nchi iliyojitenga na dunia. Hivyo, Kiingereza kama lugha ya kimataifa imelazimika kutumika katika biashara zinazozalishwa Tanzania, kwa sababu Kiingereza ndicho kilichokuwa na soko duniani. Ushahidi wa hayo unathibitishwa na bidhaa kadhaa zinazozalishwa Tanzania. Kwa mfano bidhaa zinazotengezwa Tanzania zilizotumia Kiingereza ni nyingi ukilinganisha na zile zilizotumia Kiswahili.

Mfano wa kifungashio kilichotumia lugha ya kiingereza pekee

Data hizi zimeonesha kuwa, kifungashio hiki cha bidhaa ya mchele kimetumia lugha ya Kiingereza tu. Bidhaa ambayo imezalishwa Tanzania na hutumiwa na jamii pana ya Watanzania katika maisha yao ya kila siku, kama bidhaa mama kwao. Uchambuzi matini umebaini kuwa, Utumiaji wa lugha ya Kiingereza katika vifungashio vya bidhaa ni miongoni mwa utekelezwaji wa agizo la mwongozo wa usajili wa bidhaa za chakula Zanzibar. Hivyo, vifungashio vya bidhaa vinavyotumia Kiingereza ni miongoni mwa vifungashio vilivyofuata mwongozo kwa kutekeleza maelekezo ya mwongozo huo. Kipengele namba 5.3.11 (b) cha mwongozo wa usajili wa chakula kimeweka wazi matumizi ya lugha ya Kiingereza pekee katika vifungashio vya bidhaa za ndani na hata zile zinazoagizwa kutoka nje.

'...kuwepo kwenye vifungashio vya chakula chochote kilichowekwa tayari itakuwa katika Kiswahili au Kiingereza..."

Pamoja na kuwa lugha ya Kiingereza ni lugha ya kigeni na ni lugha ya pili kwa Wazanzibari, kupitia uchambuzi matini utafiti huu umebaini kuwa, vifungashio vingi vya bidhaa hutumia lugha ya Kiingereza kuliko lugha nyingine yoyote duniani. Hii ni kutokana na hatamu ya lugha ya Kiingereza ulimwenguni. Mtafiti amechunguza vifungashio 20, 11 kati ya hivyo sawa na aslimia 55 vimetumia lugha ya Kiingereza pekee. Hali hii inaashiria matumizi makubwa mno ya lugha ya Kiingereza katika bidhaa zinazozalishwa Tanzania. Taifa ambalo jamii pana hutumia lugha ya Kiswahili katika harakati zao za maisha na biashara.

Kwa upande wa wasimamizi wa utekelezaji wa muongozo wamedai kuwa, vifungashio vya bidhaa zinazozalishwa Tanzania hutumia zaidi lugha ya Kiingereza. Hali ambayo inatokana na kuwa, lugha hiyo ni lugha ya biashara kimataifa. Wakifafanua zaidi wamedai kuwa, wafanya biashara hutumia zaidi lugha ya Kiingereza kutokana na sababu mbili kuu. Mosi, soko la ndani. Hii inatokana na kuwa Zanzibar, inakabiliwa na wageni kutoka mataifa mbalimbali, kutokana na hali hiyo, wafanya biashara hutumia lugha ya Kiingereza zaidi ili kukidhi haja kwa wageni hao. Pili, mapenzi kwa lugha ya Kiingereza. Kwa mfano, Wasimamizi wa utekelezaji wamedai kwamba,wafanya biashara hutumia lugha ya Kiingereza kwa sababu wanaipenda. Hii inatokana na kuamini kuwa, kifungashio kinachoandikwa lugha ya Kiingereza kinapendeza na kuvutia wateja. Jambo ambalo husaidia kukuza soko la biashara sambamba na kuongezeka kwa mapato.

Licha ya kuwa matumizi ya lugha ya Kiingereza katika vifungashio hivi ni sehemu ya utekelezwaji wa agizo la mwongozo juu ya kipengele cha matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa bado vina udhaifu ndani yake. Udhaifu ambao unatokana na kutumia lugha ya Kiingereza tu. Lugha ambayo ni ya kigeni na ni lugha ya pili kwa wazawa wa taifa hili. Hivyo, kifungashio hiki kimekuwa na changamoto ya ufahamikaji wake kwa watumiaji wa jamii ya Zanzibar. Watumiaji wengi wa bidhaa hii ni watu wasioelewa vyema lugha ya Kiingereza. Bidhaa hizi hutumika sana katika maisha ya kila siku. Udhaifu huu unatokana na udhaifu wa mwongozo. Mwongozo ambao haukumlazimisha mzalishaji wa bidhaa kutumia lugha ya Kiswahili ambayo inafahamika vyema na watumiaji wa bidhaa katika jamii. Hali ambayo imetokana na lugha ya Kiswahili kutopewa hadhi inayostahiki katika vifungashio vya bidhaa.

Hoja hii inatokana na msingi wa nadharia ya mazingatio ya lugha ya [13] imefafanua kuwa, lugha ni tatizo. Hivyo, kutumika kwa lugha ya Kiingereza pekee bila ya Kiswahili katika vifungashio vya bidhaa kunasababisha matatizo ya kutokufahamu maelekezo yatokanayo na bidhaa husika. Vilevile, mtaalamu huyo amedai kuwa, baadhi ya wakati lugha ya wachache huunganishwa na lugha ya wengi ambayo inazungumzwa katika eneo pana, jambo ambalo husababisha kumezwa kwa lugha ya wachache na baadhi ya wakati kupotea kabisa. Hali hii ipo kinyume katika vifungashio vya bidhaa zinazotengezwa Tanzania. Ukweli ni kuwa, vifungashio vya bidhaa zinazotengezwa Tanzania vimeimeza lugha ya wengi na ya wazawa. Jambo ambalo limesababisha vifungashio vya bidhaa vilivyotumia Kiingereza kuwa vingi kuliko vinavyotumia Kiswahili.

Matokeo ya utafiti huu yanafanana na utafiti uliofanywa na [4] ambao wameeleza kuwa, lugha za kigeni kama vile, Kijapani, Kikorea, na Kiingereza huleta athari kwenye lebo za ufungashaji wa bidhaa kuhusu namna watumiaji wanavyopendelea muonekano wa vifungashio. Muonekano huo hutoa taathira katika maeneo mbalimbali kama vile: (i) kuhamasisha umakini kwa watumiaji wa bidhaa, (ii) Hujenga uaminifu kwa watumiaji, (iii) Hutambulisha ubora wa bidhaa, (iv) Nia ya kununua bidhaa. Nadharia hii inatokana na ukweli kuwa, lugha inapotumika bila ya kufikia lengo la mawasiliano inabakia kuwa ni tatizo. Matumizi ya lugha ya Kiingereza pekee katika vifungashio vya bidhaa huwasababisha watumiaji wa bidhaa ambao ni wenyeji wa Zanzibar kukosa mambo muhimu yaliyotajwa na wataalamu hawa. Jambo ambalo huwafanya watumiaji kutokufikia malengo yao ya kufahamu maelekezo yanayotokana na bidhaa husika.

Kwa mujibu [13], kifungashio hiki, kimekuwa ni dhaifu kwa sababu lugha iliyotumika haifanikishi lengo la mawasiliano katika mazingira halisi ya jamiii husika. Tatizo ambalo limepelekea kutofikiwa kwa lengo la mawasiliano kwa watumiaji wa bidhaa hiyo. [22] ameeleza kuwa, jamii huweza kuelewana ama kutengana kupitia lugha. Akikazia hoja hiyo ameeleza kuwa, kusambaa kwa lugha ya Kiingereza kunaleta matatizo makubwa duniani kama vile, ubaguzi, na kuwanyima haki watumiaji wa lugha nyingine. Maelezo ya mtaalamu huyu yanawiana na vifungashio vya bidhaa ambavyo vimetumia Kiingereza pekee, ambapo wenyeji hushindwa kufahamu vyema maelekezo ya bidhaa husika.

Pamoja na kuwa lugha ya Kiingereza ina umuhimu katika kuleta maendeleo lakini pia imekuwa ikikandamiza na kutishia lugha za wenyeji katika nchi husika. Zaidi ya hayo, nchi ambazo Kiingereza sio lugha yao ya kwanza, wawe makini na ueneaji wa lugha ya Kiingereza duniani katika upangaji wa sera ya lugha ili wasichafue mila na tamaduni zao [24]. Jambo ambalo limesababisha zionekanwe lugha za wenyeji hazina maana mbele ya lugha ya Kiingereza. [11] ameunga mkono hoja hiyo kwa kusema kuwa, kukua na kuenea kwa lugha ya Kiingereza duniani kumeifanya lugha hiyo kuwa ndio lugha kuu ambapo lugha nyingine kutupiliwa mbali pamoja na kutokuwepo kwa usawa katika maamuzi baina ya lugha ya Kiingereza na lugha nyingine. Lugha za wenyeji zinahitaji kuboreshwa na kukuzwa ili zitumike katika mawasiliano ya kitaifa na ya kimataifa. Akizungumzia kuhusu upangaji lugha amedai kuwa, usambaaji wa lugha ya Kiingereza umechangia mipango ya kuwa na sera ya lugha katika mataifa mbalimbali duniani. Hoja ambayo, imechangia miongozo ya nchi

mbalimbali kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza pamoja na kupewa kipaumbele kwa lugha hiyo katika upangaji sera wa nchi hizo. Hali ambayo inadhihirika katika vifungashio vya bidhaa zinazotengezwa Tanzania.

Ni wazi kuwa, kusambaa kwa lugha ya Kiingereza kumechangia mwongozo wa usajili kuweka hadhi sawa lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Kitendo hichi kimejenga udhaifu kwa mwongozo. Jambo ambalo limesababisha udhaifu katika vifungashio vya bidhaa ambavyo vimekosa lugha ya wazawa ya Kiswahili. Lugha ambayo inafahamika kwa urahisi na wenyeji. Licha ya kuwa, Kiingereza ni lugha kuu ya biashara duniani bado mwongozo wa usajili wa chakula una nafasi ya kulazimisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika vifungashio vya bidhaa zinazotayarishwa Tanzania. Hii ni kutokana na hadhi ya lugha ya Kiswahili kwa jamii ya Watanzania. Kutokana na wataalamu hao utafiti umebaini kuwa, Licha ya kuwa, vifungashio vilivyoandikwa Kiingereza ni sehemu ya utekelezwaji wa kipengele cha matumizi ya lugha katika mwongozo wa usajili wa bidhaa za chakula, vifungashio hivyo ni dhaifu kutokana na kukosekanwa kwa lugha ya Kiswahili kulingana na watumiaji wengi wa bidhaa hiyo.

4.3 UTUMIAJI WA LUGHA YA KISWAHILI NA KIINGEREZA KATIKA VIFUNGASHIO VYA BIDHAA ZA CHAKULA

Utumiaji wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika vifungashio vya bidhaa ni miongoni mwa maelekezo ya mwongozo wa usajili wa chakula Zanzibar. Baadhi ya bidhaa zimebainika kutumia Kiswahili na Kiingereza kama takwa la kutekeleza agizo lililokuwepo katika mwongozo wa usajili wa chakula. Kwa sababu, mwongozo wa usajili wa chakula wa Zanzibar umeruhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Hii ni kutokana na sababu kadhaa zinazohusiana na mahitaji ya kisheria, kibiashara, na kijamii.

Kiswahili ni lugha ya kitaifa nchini Tanzania na Zanzibar, na hutumika sana katika mawasiliano ya kila siku hususan katika elimu, biashara, vyombo vya habari, vyombo vya kutunga sharia, mahakama, pamoja na shughuli za kijamii. Aidha, Kiswahili ni lugha muhimu kwa kutoa maelekezo ya bidhaa hususan kwa wateja wa ndani. Kwa upande wa Kiingereza, ni lugha ya kimataifa inayotumika sana katika soko la biashara, elimu, na utalii. Zanzibar, kama kisiwa chenye utalii mkubwa na biashara ya kimataifa, ni vyema kutoa maelezo ya bidhaa kwa Kiswahili na Kiingereza ili pia kuwahudumia watalii na wageni waliopo nchini.

Data ifuatayo inaonesha matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika vifungashio vya bidhaa za chakula.

Kifungashio chenye mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza

Data hii inaonesha kuwa, ndani ya jamii ya watu wa Zanzibar vipo vifungashio vinavyotumia sambamba lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa kutumia mbinu ya uchambuzi matini utafiti umebaini kuwa, vifungashio vilivyotumia Kiswahili na Kiingereza vimefuata kikamilifu maelekezo juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa. Kwa mujibu wa mwongozo vifungashio vya bidhaa za chakula vinaweza kutumia sambamba lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Hali hiyo inathibitika pale mwongozo uliposema. "... au Kiswahili na Kiingereza..."

Kwa vile, vifungashio hivyo vimetumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza ni wazi kuwa, vifungashio hivyo vimetekeleza masharti ya ufungashaji wa bidhaa Zanzibar. Kutokana na hali hiyo, vifungashio hivi vimekuwa na ubora kutokana na kufuata maelekezo ya mwongozo huo. Aidha, ubora wa vifungashio hivyo, unatokana na ubora wa mwongozo ambao umeruhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa pamoja.

Kulingana na maelekezo ya mwongozo, lugha ya Kiswahili na Kiingereza zimepewa umuhimu wa kipekee katika vifungashio vya bidhaa. Hali hii inatokana na hadhi ya lugha hizi kwa jamii. Kupitia mbinu ya uchambuzi matini vifungashio vitatu kati ya 20 sawa na 15% vimebainika kutekeleza maagizo ya mwongozo kwa kutumia lugha ya Kiingereza na Kiswahili kwa pamoja. Zaidi ya hayo, vifungashio hivyo vimekuwa bora kutokana na kuzingatia lugha ya Kiswahili ambayo ni ya kwanza na ya taifa. Vile vile, lugha ya Kiingereza ni lugha ya pili na ni lugha rasmi kwa jamii ya Wazanzibari. Lakini pia, ni lugha kuu ya biashara duniani. Kutokana na hali hiyo, vifungashio hivi vina uzito wa maana kwa Wazanzibari na wageni

Maelezo hayo yanafanana na mawazo ya [13] pale aliposema kuwa, lugha ni rasilimali na ni haki ya kila mtu. Matumizi ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili katika vifungashio vya bidhaa ni ishara ya utumiaji mzuri wa rasilimali hizi kwa wenyeji na wageni. Hii ni kutokana na lugha hizi hutumiwa na jamii pana ukilinganisha na lugha nyingine. Hivyo, vifungashio vya bidhaa vinavyotumia Kiswahili na Kiingereza hufahamika na watu wengi zaidi ukilinganisha na vifungashio vyengine. Aidha, matumizi hayo, yamepelekea watumiaji wengi wa bidhaa, kupata haki zao kwa kufahamu maelekezo ya vifungashio vya bidhaa za chakula.

Matumizi haya ya lugha katika vifungashio vya bidhaa yanaunga mkono matokeo ya utafiti wa [23] na [19] ambao wamefafanua kuwa, vifungashio vya bidhaa hutumia sambamba lugha za wenyeji na wageni sio tu kwa lengo la kutafuta soko bali pia ni sehemu ya utekelezwaji wa sera husika. Jambo ambalo husaidia jamii pana kufahamu maelekezo ya bidhaa. Hatua ambayo ina mchango mkubwa katika kuinua soko la ndani na nje la bidhaa husika. Maelezo haya yanakwenda sambamba na utafiti uliofanywa na [5] na [22] ambao waligundua kuwa, bidhaa zinazouzwa zinazotoka katika viwanda vingi duniani zinasaidia kushika hatamu kwa lugha ya Kiingereza ameongezea kuwa, Kiingereza kinasalia kuwa lugha kuu ya biashara na maisha ya umma. Matumizi ya lugha ya Kiingereza yana umuhimu mkubwa kimataifa katika soko la biashara duniani. Jambo ambalo huwawezesha watu mbalimbali kuweza kufahamu maelekezo ya bidhaa husika. Tafiti hizi zinawiana na utafiti wa [9] ambao umegundua mchango wa lugha ya kigeni katika kifungashio chenye lugha ya nchi mwenyeji. Mtaalamu huyu amedai kuwa, lugha ya kigeni husaidia kupanua soko la bidhaa za ndani na hata nje pale inapotumika sambamba na lugha ya wenyeji kutoka nchi husika.

Hoja hii inatiliwa mkazo na [22] pale aliposema bidhaa zinazotoka katika viwanda ambavyo Kiingereza si lugha yao mama husaidia kusambaa kwa lugha ya Kiingereza. Zaidi ya hayo, amesema kuwa, lugha ni chombo cha utu, heshima, na majivuno. Usambaaji wa lugha ya Kiingereza ulimwenguni kumepelekea lugha hiyo kutumika katika nyanja mbalimbali kama vile, elimu, uchumi, siasa utamaduni, ufundi na mitandao kwa nchi zinazozungumza Kiingereza na zisizozungumza Kiingereza. Utumiaji wa lugha ya Kiswahili katika vifungashio vya bidhaa za Tanzania ni jambo muhimu sana katika kufikia malengo ya kufahamu maelekezo mbalimbali yatokanayo na bidhaa husika [1].

Utumiaji wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili katika vifungashio vya bidhaa ni utumiaji mzuri wa rasilimali kitaifa na kimataifa katika soko la biashara na utandawazi. Ruiz (1984) amedai kuwa, lugha ni rasilimali muhimu inayowaunganisha watu na mataifa mbalimbali duniani. Lugha ya Kiingereza imefanikiwa kuyaunganisha mataifa mbalimbali katika soko la biashara. Vilevile, lugha ya Kiswahili ni lugha pekee iliyofanikiwa kuwaunganisha Watanzania.

Pia, kwa upande wa [11] anaeleza kuwa, ukubwa na hadhi ya lugha ya Kiingereza umeimarika kiasi ambacho inastahiki kutumiwa na dunia nzima bila ya kupingwa. Hoja hii imeshadidiwa na [5] pale aliposema kuwa, pamoja na kuwa lugha ya Kiingereza kuwa ni lugha ya kimataifa lakini pia, ni lugha kuu ya biashara na maisha ya umma. Hii ni kutokana na nguvu ya lugha ya Kiingereza katika soko la biashara duniani.

Maelezo yaliyotangulia yanaonesha kuwa mataifa mbalimbali hutumia lugha zao za asili na za wenyeji kama ni sehemu ya utekelezwaji wa sera ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula. Katika utekelezaji huo, matumizi ya lugha ya Kiswahili sambamba na lugha ya Kiingereza ni muhimu sana kutokana na uhalisia wa mazingira ya Zanzibar kitaifa na kimataifa. Hivyo, ubora wa vifungashio hivi unatokana na kule kuwa kibebeo cha haki na maisha ya walio wengi, Zanzibar.

5.0 VIFUNGASHIO VYA BIDHAA AMBAVYO HAVIKUTEKELEZA AGIZO LA MUONGOZO

Kwa mujibu wa mwongozo, vifungashio vilivyokuwa havikufuata mwongozo ni vifungashio ambavyo vimetumia lugha za kigeni pekee ukitoa lugha ya Kiingereza. Rejea kipengele namba 5.3.11 (b) katika mwongozo wa usajili wa chakula.

Kwa mujibu wa watoa taarifa, kumejitokeza madai kuwa ukiukwaji wa mwongozo husababishwa na mambo matatu makuu. Mosi udanganyifu kwa wafanya biashara. Jambo hili hutokea pale mfanya bishara anapoficha bidhaa ambazo vifungashio vyake havikufuata mwongozo wa usajili na kuzionesha bidhaa ambazo vifungashio vyake vimefuata mwongozo husika. Pili, baadhi ya wafanya biashara hawausomi mwongozo husika. Tatu, baadhi ya wafanya biashara hawahudhurii katika mafunzo ambayo hutolewa rasmi na wasimamizi wa utekelezaji wa mwongozo ikiwa ni miongoni mwa hatua za utekelezaji wa mwongozo. Kutokana na hoja hizi vifungashio vya bidhaa vilivyokiuka maagizo ya mwongozo vimejitokeza ingawa kwa uchache sana.

5.1 VIFUNGASHIO AMBAVYO HAVIKUTUMIA LUGHA YOYOTE

Vifungashio vya bidhaa ambavyo havikutumia lugha yoyote ni vifungashio ambavyo havikutekeleza agizo na masharti ya ufungashaji Zanzibar. Mwongozo wa usajili wa chakula wa Zanzibar, haukutoa fursa kwa wafanya biashara ya kutokuandika maelekezo katika vifungashio vya bidhaa yoyote. Kwa mujibu wa mwongozo wa usajili wa chakula vifungashio vya bidhaa ni lazima kutumia lugha ya Kiswahili au Kiingereza au Kiswahili na Kiingereza au lugha nyingine yoyote pamoja na Kiswahili au Kiingereza.

"...kuwepo kwenye vifungashio vya chakula chochote kilichowekwa tayari itakuwa katika Kiswahili au Kiingereza au Kiswahili na Kiingereza, au lugha nyingine yoyote pamoja na Kiswahili au Kiingereza"

Maelezo haya hayakutoa fursa kwa wazalishaji wa bidhaa kuweka bidhaa zao sokoni bila ya kuwekwa maelekezo katika vifungashio vya bidhaa husika. Kutokana na hoja hii ni wazi kuwa, vifungashio vya bidhaa ambavyo havikuandikwa havikutekeleza agizo la mwongozo wa usajili wa chakula Zanzibar.

Baadhi ya vifungashio vinavyokiuka mwongozo kwa kutotumia lugha yoyote katikavifungashio vya bidhaa

Data hii inaonesha kuwa, vifungashio hivi vya bidhaa havikutumia lugha kabisa. Kupitia mbinu ya uchambuzi matini utafiti umebaini kuwepo kwa bidhaa ambazo hazikuandikwa lugha yoyote katika vifungashio vyake. Bidhaa hizo aghlabu ni zile zinzotengenezwa ndani ya Tanzania. Hali hii inadhihirisha wazi kuwa, baadhi ya wajasiriamali hawatekelezi maagizo halali ya muongozo wa usajili wa chakula juu ya matumizi ya lugha katika vifingashio vya bidhaa. Hivyo, ni wazi kuwa vifungashio hivyo ni dhaifu, udhaifu ambao unatokana na kutokufuata maelekezo ya muongozo. Vile vile, vifungashio hivyo ni dhaifu mno kwa vile, watumiaji wa bidhaa hawapati fursa ya kufahamu chochote kuhusu bidhaa husika. Vifungashio vinne kati ya 20 havikutekeleza agizo la mwongozo wa usajili, wa chakula juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa. Uchambuzi matini umetofautiana na baadhi ya taarifa kutoka kwa wasimamizi wa utekelezaji wa mwongozo ambapo wamedai kuwa, vifungashio visivyotumia lugha yoyote havipo Zanzibar. Jambo ambalo ni kinyume na uhalisia ulivyo. Uchunguzi matini umegunduwa kuwa, miongoni mwa bidhaa ambazo vifungashio vyake havikutumia lugha yoyote ni kama vile, ubuyu, njugu, ukwaju, na korosho. Matokeo ambayo

yamekwenda sambamba na baadhi ya watoa taarifa kutoka mamlaka husika. Vifungashio kama hivyo ni wazi kuwa, huwapa shida watumiaji wa bidha kujuwa maelekezo mbalimbali yatokanayo na bidhaa husika. Maelekezo hayo, ni yale yanayotokana na matumizi, uhifadhi, viambata vilivyomo, muda wa kutumia bidha, jina la bidhaa, kampuni inayotengeza bidhaa husika na mengineyo.

Kwa mujibu wa [13] lugha ni rasilimali, lugha ni haki na lugha hiyo hiyo huweza kuwa tatizo. Kutokana na vifungashio hivi kutoandikwa lugha yoyote ni wazi kuwa rasilimali lugha haikutumika. Jambo ambalo limesababisha watumiaji wa bidhaa kukosa haki yao ya kufahamu maelekezo. Kwa mantiki hiyo, hali hii husababisha matatizo ya kutokufahamu chochote kwa watumiaji wa bidhaa hizo. Kwani kupitia lugha mtumiaji wa bidhaa hupata kufahamu matumizi, uhifadhi, kuharibika kwa bidhaa, viungo vilivyotumika na mengineyo. Hivyo, ni wazi kuwa vifungashio hivi ni dhaifu mno ukilinganisha na vifungashio vyote vilivyoashiria kuwa dhaifu katika utafiti huu. Hii ni kutokana na kuwa, vifungashio vya bidhaa hizi havina msaada wowote juu ya kufahamu maelekezo kwa watumiaji wa bidhaa hizo.

Wataalamu mbalimbali wamezungumzia umuhimu wa matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa. Miongoni mwao ni [10] na [18] wamesema kuwa, ni vyema wafanya biashara kutumia lugha zinazotumiwa na jamii pana ndani ya nchi, ili kujenga uaminifu wa bidhaa kwa wateja. Hoja hii inamaanisha kuwa, bidhaa ambayo inatumia lugha ambayo wananchi hawaifahamu ni vigumu kufaidika na bidhaa hiyo. Sambamba na hali hiyo bidhaa ambazo hazikuandikwa kabisa matokeo yake yanafanana na bidhaa ambazo hutumia lugha ambazo hazifahamiki na jamii husika.

[3]wamesema, wataalamu na wasomi wanakubaliana kwamba ufungashaji ni dhana ya mawasiliano ambayo huathiri mafanikio ya uuzaji. Kitendo cha wafanya biashara kuingiza bidhaa sokoni bila ya kutumia lugha ni ukiukwaji wa kanuni za mwongozo. Aidha, bidhaa ambazo zimekosa lugha ni wazi kuwa athari yake huwa kubwa zaidi kwa vile mtumiaji hapati fursa ya kufahamu chochote kutokana na bidhaa hiyo.

Vilevile, [20] ameeleza kuwa, mpango lugha ni mikakati inayowekwa kulingana na tabia ya lugha. Pia, ameeleza kuwa, upangaji lugha ni ule upangaji wa tabia ya lugha kwa mujibu wa matumizi mbalimbali ya lugha katika jamii. Upangaji huo, hupanga namna ya kudhibiti matumizi ya lugha katika jamii na hautoi fursa kwa watumiaji wa lugha kutumia kinyume na maamuzi yaliyofikiwa na mamlaka husika. Kutokana na hoja hii ni wazi kuwa, vifungashio hivi vimekwenda kinyume na maamuzi ya mamlaka husika. Jambo ambalo limechangia udhaifu wa vifungashio hivyo. Akifafanua zaidi amedai kuwa, mara nyingi huwa kuna muwachano baina ya itikadi na utekelezaji wa sera na miongozo inayowekwa juu ya matumizi ya lugha katika mataifa mengi duniani. Hali hii inadhihirika katika vifungashio vya bidhaa za chakula, pale wafanya biashara wanapoingiza bidhaa sokoni ambazo vifungashio vyake havikuandikwa chochote.

Matokeo ya utafiti huu yanakwenda sambamba na utafiti uliofanywa na [14] ambao umefafanua kuwa sera ya lugha ni chombo kinachoongoza sheria, kanuni, na taratibu za matumizi ya lugha zinazokusudiwa kufikia maendeleo ya lugha zilizopangwa katika jamii. Kuwepo kwa sera ya lugha

hupelelekea kufanyika tathmini ya uhakika ya maendeleo ya matumizi ya lugha. Tathmini ambayo imemsaidia mtafiti kubaini vifungashio vya bidhaa ambavyo vinatekeleza agizo la mwongozo na vile ambavyo vinakiuka agizo la mwongozo wa usajili wa chakula wa Zanzibar.

Makala hii imetathmini utekelezaji wa mwongozo wa usajili wa bidhaa za chakula, juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa hizo. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa, vifungashio vya bidhaa ziliopo Zanzibar katika utekelezwaji wa mwongozo huo hutumia lugha ya Kiswahili pekee, Kiingereza pekee pamoja na Kiswahili na Kiingereza kwa pamoja. Vifungashio 16 kati ya 20 vilivyochunguzwa ambapo ni sawa na 80% vimetekeleza agizo la mwongozo juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula. Aidha, vifungashio vilivyogundulika ambavyo havikutekeleza agizo la mwongozo ni vinne kati ya 20 sawa na asilimia 20%. Vifungashio vilivyogundulika ambavyo havikufuata mwongozo ni vile ambavyo havikutumia lugha yoyote. Zaidi ya hayo, utafiti huu, haukugundua utekelezwaji wa vifungashio ambavyo vimetumia lugha ya Kiswahili sambamba na lugha nyingine za kigeni, na vifungashio vilivyotumia lugha ya Kiingereza sambamba na lugha nyingine za kigeni katika mazingira ya Zanzibar kwa bidhaa zinazotengezwa Tanzania.

6. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Kwa ujumla makala hii imetathmini utekelezaji wa mwongozo wa usajili wa chakula juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula. Kupitia uchunguzi uliofanyika, matokeo yameonesha kuwa, kipengele cha matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula kinatekelezwa kwa kiasi kikubwa. Aidha, wapo wajasiriamali wachache ambao hawatekelezi maelekezo ya mwongozo wa usajili wa chakula juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za chkula. Jambo ambalo, limesababisha baadhi ya bidhaa kuingizwa sokoni bila ya kuzingatia matumizi ya lugha.

Aidha, utafiti umegundua kuwa, vifungashio vya bidhaa za chakula vilivyotumia Kiswahili ni vichache licha ya kuwa lugha ya Kiswahili ndio lugha inayofahamika kwa asilimia 99 ya Watanzania. Hali ambayo inatokana na mwongozo wa usajili wa chakula kuweka lugha ya Kiswahili kuwa mbadala wa lugha ya Kiingereza katika vifungashio vya bidhaa. Zaidi ya hayo, kushika hatamu kwa lugha ya Kiingereza duniani kumepelekea matumizi makubwa ya lugha ya Kiingereza katika vifungashio vya bidhaa zinazotengezwa ndani ya jamii ya Watanzania. Kulingana na matokeo ya utafiti makala hii inapendekeza kuwa, wasimamizi wa utekelezaji wa mwongozo husika kuchukua juhudi za makusudi kutoa elimu ya kutosha kwa watengezaji wa bidhaa na wafanya biashara juu ya umuhimu wa kufuata maagizo ya miongozo ya serikali pamoja na umuhimu wa matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula. Sambamba na hilo, kuwachukulia hatua wale wote ambao wanakiuka maagizo ya utumiaji wa lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula. Hatua ambayo inaweza kusaidia uboreshaji katika utekelezwaji wa mwongozo husika.

MAREJEO

Abdallah, S. (2018). Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika bidhaa za watoto Nchi Tanzania: Yaliyokuwemo na Yasiyokuwemo. Jarida la Mwanga.Vol.2(2)1https://journals.mu.ke/ndex.php/mwl/article/vew/88.

[1] Bodomo, A. (1996). Language for Sustainable Development in Africa. Department of Linguistics, Norwegian University of Science and Technology. Trondheim.

[2] Charinsarn, A. & Wagnner, U. (2020). "What language should be displayed on product packaging? How unconventional lettering influences packaging and product evaluation". Journal of International Consumer Marketing 33 (5):1-18. DOI:10.1080/089615302020.17417483.

[3] Han-Chiang Ho, Candy Lim Chiu, Dai Jiang, Jiale Shen & Hong Xu (2019). Influence of Language of Packaging Labels on Consumers' Buying Preferences, Journal of Food Products Marketing, DOI: 10.1080/10454446.2019.1572562. https://doi.org/10.1080/10454446.2019.1572562

[4] Heugh, K, (1999). Languages, development and reconstructing development in South Africa. International Journal of Educational Development 19, 301–31

[5] Hornikx, J., & Starren, M. (2006). The relationship between the appreciation and the comprehension of French in Dutch Advertisements. In R. Crijns & C. Burgers (Eds.), Werbestrategien in Theorie Und Praxis, Sprachlıche Aspekte Von Deutschen UndNiederländıschen Unternehmensdarstellungen Und Werbekampagnen (pp. pp. 129–145).

[6] Institute of Export of America. (2022). Language & localization in packaging and labelling for export. https://open toexport.com.

[7] Khan, H., & Lee, R. (2020). A sociolinguistic perspective of the effects of packaging in bilingual markets. Journal of Brand Management, 27(2), 130-142.

[8] Maack, V. H, na Schwenk, J. (2016) Effects of multillingual product on product attitude, perceived quality, and taste perceptions. Katika kitabu: Advances in Advertising Research. (Vol.V1) (pp.351-363). DOI:10.1007/978-3-658-10558-7 – 27

[9] Patison, E. (2018). "Why language is crucial to succeeding in new markets". https://www.marketingweek.com

[10] Phillipson R (1992) Linguistic imperialism (1st edn.). Oxford University Press.

Rais, A. S., Onyango, J. & Mbaabu, I. (2022). Tathmini ya Uamilifu wa Kiswahili Nchini Uganda: Mintarafu, Ueneaji wa Matumizi Yake Kwenye Asasi ya Uchapishaji. East African Journal of Swahili Studies, 5(1), 73- 83. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.641.

[11] Ruiz, R. (1984). Orientation on language planning. NABE Journal, 8(2), 15-34.

[12] Rubin, J., & Jernudd, B. H. (Eds). (1971). Can language be planned? Sociolinguistic theory and practice for developing nations. Honolulu: University of Hawai'i Press.

[13] Run, E. C. D., & Chin, S. F. (2006). Language use in packaging: The reaction of Malay and Chinese consumers in Malaysia. Sunway Academic Journal, 3, 133-145.

[14] Salem, M. (2024). Local language use in packaging and its impact on the Palestinian consumers' purchase decision. In: Alareeni, B., Elgedawy, I. (eds) AI and Business, and Innovation Research: Understanding the Potential and Risks of AI for Modern Enterprises. Studies in Systems, Decision and Control, vol 440. Springer, Cham. https://doi.org/10.1007/978-3-031-42085-6_51.

[15] Sovu, A. Y. (2021). Changamoto za uingizwaji wa masuala yahusuyo lugha katika sera za elimu na utamaduni: Haja ya kuwa na sera mahususi ya lugha Tanzania Jarida la Mnyampala–Juz. Na. 2/1 95

[16] Shngkuan, M. (2022). The business benefits of learning a new language. Entrepeneur.https://www.entrepreneur.com/growing-a-business/thebussiness-benefits-learning-a-new- language/ 4232718.

[17] Shen, Q. (2021). Research on the application of regional cultural visual language in the packaging design of local specialties. In The 6th International Conference on Arts, Design and Contemporary Education (ICADCE 2020) (pp. 649-652). Atlantis Press.

[18] Shohamy, E. (2006). Language Policy: Hidden agendas and new approaches. Routledge.

[19] Spolsky, B. (2004). Language Policy. Combridge. Combridge University Press.

[20] Tsuda, Y. (2008) English hegemony and English devide. China Media Research. Volume 4 (1) 2008. University of Tsukuba, Japan.

[21] Uyar, A. (2018). A Study on Consumers' Perception About Chinese Products and Their Willingness to Buy, International Journal of Eurasia Social Sciences, Vol: 9, Issue: 32, pp. (1121-1143).

[22] Zeng, J. & Yang, J. (2024). English language hegemony: retrospect and prospect. Humanities & Social Sciences Communication.https://doi.org/10.1057/41599-024-02821-z.Gordin, MD. (2015). Scientific Babel: how science was done before and after global English. University of Chicago Press.